

## **Lack of Respect for Teachers**

### **Swahili transcript:**

Mtoa mada: Kwa hiyo serikali inapata changamoto kubwa kwamba ijenge shule chache lakini kubwa na za maana ambazo zinaweza zikakusanya watu toka sehemu mbalimbali nchini zikaweka Na vilevile kuhusiana na, watu wengi wamekuwa wakiukimbilia ualimu, kama alivyosema hapa mwenzangu hapa Willy, kwamba tunaenda kwenye ualimu baada ya kuona sasa sehemu zote za maisha zimefunga. Lakini ni sababu tu kwamba mishahara ya walimu iko chini sana, na vijana wakishapata elimu wanaangalia zile kazi ambazo zina mshahara mkubwa, na heshima ya kazi inategemeana na mshahara. Kwa ufupi, kipindi cha nyuma, kazi ambayo ilikuwa na heshima kubwa wakati tunapata uhuru ilikuwa ni kazi ya ualimu. Kwa sababu mzungu alichokifanya ni kwamba, kwa sababu alikuwa anajua kwamba akiruhusu wataanzania au waafrika tufundishane sisi kwa sisi, tutaibua hali ya uzalendo, kwa hiyo kazi ya ualimu ilikuwa chini ya mzungu mwenyewe, sisi akatupatia kazi nyingine; na wa sababu yeye ndio alikuwa anafundisha, akajitengea mshahara mkubwa sana. Ilikuwa njia ya namna gani, ya kutumia hela zetu katika hali ya kushirikishana, kwa hiyo yeye akajipa kazi ya ualimu na akaongeza mshahara mkubwa. Kwa hiyo sasa raisi wa kwanza alipoingia, mwalimu nyerere akauchukua ule utaratibu kama ulivyo. Kwa hiyo hata walimu wa mwanzo kabisa wazalendo nao bado walikuwa wanalipwa mshahara mkubwa, kwa hiyo watu wengi wakakimbilia kule kwenye ualimu, na kweli mtu akisema mimi mwalimu, anaheshimika. Na watu wote waliokuwa wanafanya vizuri katika taaluma ndio walikwenda kuwa walimu, kwa sababu ilikuwa ndio kazi yenye mshahara mkubwa na yenye thamani kubwa, kwa sababu ndio kazi aliyokuwa anafanya mzungu mwenyewe na akaiacha. Sasa baadae, baada ya kuingia raisi wa awamu ya pili, ule mfumo ulibadilika. Vile vitu mbalimbali alivyokuwa akivipata mwalimu vikapotea vyote. Kwa hiyo ndio ikawa kazi yenye kipato cha chini kuliko zote. Kwa hiyo watu walipoona hivyo, wakaanza kuikimbia, kwa hiyo mpaka mtu akishindwa ndio aje kuwa mwalimu. Kwa hiyo serikali ina changamoto ya kuithamini tena kazi ya ualimu, na itaithamini kama itakuza kipato cha walimu. Kama kwenye upande wa walimu mshahara utakuwa ni mkubwa, maana yake hata mimi nitapenda nikasomee ualimu nije kufanya kazi na kuwa na maisha mazuri. Na kwa wale watu wote wanaofaulu vizuri katika nchi pia wataenda kwenye ualimu kwa sababu ni mahali ambapo pana pato zuri

### **English translation:**

Presenter: The government has a challenge to make sure that they build schools that are big enough and have good facilities and teachers. After all other alternatives in their lives have failed; there are many people who want to be teachers, as my friend Willy has stated. Many people decide to become teachers after failing to get good paying jobs. Teachers are paid low salaries, and the person's status depends on the salary she or he gets. Many young people want well-paid jobs after getting their education.

After getting our independence, teaching was a well-paid job. The colonizers knew that if they gave teaching jobs to Tanzanians or to Africans, they would establish a sense of patriotism. Teaching jobs were given to the colonizers, and they gave us other jobs. And they paid themselves a big salary. So when the first president came to power, he continued that system as it was. That's why the first teachers were paid good salaries, and many people wanted teaching jobs. During that time, if someone said "I am a teacher," she or he was respected. All the people who did well in their fields became teachers, because teaching was a well-paid job and a job with great respect.

When the second president came to power, the system changed. A teaching job became one with a low salary and without respect. As I mentioned earlier, the status of a person depends on the job a person is doing. So when people saw that the status of teaching was in decline, they no longer pursued it. The government ought to make sure they retain the status of teaching by increasing the teachers' salaries. That means that if the salary is good, even I will go to a teachers' college to become a teacher and get a good salary and have a good life. And all who perform well in their studies all over the country would love to become teachers because teaching pays well.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated